TANGAZO LA SERIKALI NA. 192 la tarehe 21/3/2025

SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE,
(NA. 13 YA 2023)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 35)*

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA BIMA YA AFYA KWA WOTE ZA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 809 la 2024

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote za Mwaka 2024 ambazo katika Kanuni hizi zinarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 2

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 2 kwa kufuta tafsiri ya msamiati "Mfuko" na kuiandika upya kama ifuatavyo:

""Mfuko" maana yake ni akaunti ya fedha za kugharamia watu wasio na uwezo kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 25 cha Sheria.".

Marekebisho ya kanuni ya 9

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 9 kwa kufuta kanuni ndogo ya (2) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(2) Skimu ya bima ya afya isiyoridhishwa na kusudio la kufutiwa usajili inaweza, ndani ya siku tisini za notisi, kuwasilisha utetezi wake wa maandishi kwa Mamlaka, na Mamlaka, ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kupokea utetezi, itatoa uamuzi kabla ya kufuta usajili.".

Marekebisho ya Kanuni ya

4. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 13 na kuiandika upya kama ifuatavyo:

*Tangazo la Serikali Na. 192 (Linaendelea)*

13

"Utaratibu wa utambuzi wa watu wasio na uwezo

13.-(1) Kwa madhumuni ya ujumuishaji wa watu wasio na uwezo katika mfumo wa bima ya afya, Wizara kwa kushirikiana na mamlaka za utambuzi itaandaa mwongozo utakaobainisha vigezo vya utambuzi wa watu wasio na uwezo.

(2) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa kanuni hii, Wizara itaziomba mamlaka za utambuzi wa watu wasio na uwezo kutambua na kuwasilisha kwake, katika muda utakaobainishwa, taarifa zinazohusiana na watu wasio na uwezo.

(3) Mamlaka za utambuzi zitafanya utambuzi wa watu wasio na uwezo kwa kuzingatia vigezo vilivyobainishwa katika mwongozo wa utambuzi wa watu wasio na uwezo na kuwasilisha taarifa kwa Wizara.

(4) Wizara mara baada ya kupokea taarifa kutoka kwa mamlaka za utambuzi chini ya kanuni ndogo ya (3), itajumuisha orodha ya watu wasio na uwezo waliotambuliwa katika kanzidata ya watu wasio na uwezo kwa ajili ya kugharamiwa bima ya afya.

(5) Wizara inaweza, pale itakapohitajika na kwa namna itakayoona inafaa, kufanya uhakiki wa taarifa za watu wasio na uwezo zilizojumuishwa katika orodha ya watu wasio na uwezo.".

Marekebisho ya kanuni ya 15

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 15 kwa kufuta kanuni ndogo ya (3).

Marekebisho ya kanuni ya 16

6. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 16(4) kwa kufuta maneno "walichogharamiwa kupitia Mfuko" na badala yake kuweka maneno "ya huduma muhimu".

Marekebisho ya kanuni ya 18

7. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 18(1)(b) kwa kuongeza maneno "kwa kuzingatia miongozo ya utoaji huduma kwa vituo vya kutolea huduma za afya;" mara baada ya neno "afya".

Marekebisho ya kanuni ya 24

8. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 24 kwa-

(a) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (1) kanuni ndogo mpya ifuatayo:

"(2) Skimu ya bima ya afya itamjulisha mwanachama kwa maandishi, kuhusu uanachama wake kufikia ukomo kwa sababu za kushindwa kuchangia, mwezi mmoja kabla ya kufikia ukomo."; na

(b) kupangilia upya kanuni ndogo ya (2) kuwa kanuni ndogo ya (3).

Kufuta na kuandika upya kanuni ya 25

9. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 25 na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Ukomo wa mtegemezi

25.-(1) Kwa kuzingatia kifungu cha 3 cha Sheria, mtegemezi atafikia ukomo endapo mwanachama atafariki au kufanya mabadiliko ya mtegemezi huyo.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), mtegemezi ambaye ni mtoto wa mwanachama wa kuzaa, kuasili au wa kambo, au ndugu wa damu wa mwanachama, atafikia ukomo wa utegemezi endapo atafikisha umri wa miaka ishirini na moja.".

Marekebisho ya kanuni ya 30

10. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 30 kwa kuongeza kivuo mwishoni mwa kanuni ndogo ya (2) kama ifuatavyo:

"Isipokuwa kwamba, skimu ya bima ya afya ya binafsi inaweza, katika kitita cha mafao ya huduma muhimu, kutoa dawa zilizoandikwa kwa majina ya kibiashara endapo zimekidhi vigezo vya kiufanisi na

*Tangazo la Serikali Na. 192 (Linaendelea)*

kiusalama.”.

Marekebisho ya kanuni ya 33

11. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 33(1) kwa kuongeza maneno “na isipokuwa katika mazingira ya dharura” mara baada ya neno “Sheria”.

Marekebisho ya kanuni 37

12. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 37 kwa kufuta kanuni ndogo ya (2).

(b) kupangilia upya kanuni ndogo ya (3) kuwa kanuni ndogo ya (2) na kanuni ndogo ya (4) kuwa kanuni ndogo ya (3).

Marekebisho ya kanuni ya 39

13. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 39 kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (4) kanuni mpya ifuatayo:

> “(5) Endapo Mamlaka itaamua kuwasilisha malalamiko kwa msuluhishi itamtaarifu mlalamikaji kwa maandishi kuhusu uamuzi huo”.

Marekebisho ya kanuni ya 46

14. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 46 kwa kufuta maneno “kulipa faini isiyopungua shilingi milioni kumi na isiyozidi shilingi milioni hamsini” na badala yake kuweka maneno “kwa adhabu kama ilivyoainishwa katika Sheria”.

Marekebisho ya Jedwali

15. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Jedwali katika Sehemu B ya Fomu Na. 2 kwa kufuta kifupi “FIU” kilichopo katika kipengele 2(c)xxv na badala yake kuweka maneno “Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu”.

Dodoma,
19 Machi, 2025

JENISTA J. MHAGAMA
*Waziri wa Afya*